

## **MKRISTO NI....**

Watu huongelea kuwa Wakristo, lakini mtu asemapo ni Mkristo hasa humaanisha nini?. Ili kurahishisha maana yake, Mkristo ni mtu aliye kama Kristo. Walakini tukichunguza maandiko katika Agano Jipy, tutapata maelezo yaliyoainishwa kwa kina jinsi alivyo Mkristo. Hili litatusaidia zaidi ili tuwe na uelewa bora wa kile tunachotamani kuwa.

**MKRISTO NI MWANA WA MUNGU**-Sifa ya kwanza tuionayo kwenye maandiko ni kwamba Mkristo wa kweli ni mwana wa Mungu. Kwa mujibu wa Yohana, waaminio wanapewa uweza wa kufanyika wana wa Mungu (Yohana 1:12; 1 Yohana 3:1,2). Fikra iliyopo hapa ni kwamba, anayefanyika kuwa Mkristo ni mwana wa Mungu ikiwa ni wa kiume ama wa kike. Ndani ya Agano Jipy, Mungu anatazamwa kama Baba wa haki (Mathayo 6:9). Kwa sababu ya kuwa na mtazamo wa hili, twapaswa kila siku kuishi kama wana wa Mungu

**MKRISTO NI MRITHI WA MUNGU**-Sifa ya pili tuionayo ni kwamba Mkristo wa kweli wa Agano Jipy ni mrithi wa Mungu. Kwa mujibu wa mtume Paulo, sisi tu warithi wa Mungu, na warithi pamoja na Kristo (Warumi 8:16,17). Kwa kuwa tu warithi pamoja na Kristo, ni lazima tushiriki katika mateso yake, na tufanyapo hivyo, tutashiriki katika utukufu wake halikadharika.

Kama wana na warithi wa Mungu tu zaidi ya watumwa. `Sisi siyo watumwa tena kama walivyokuwa Wayahudi (Wagalatia 4:6,7). Kama wana na warithi wa Mungu baraka zote zitokazo kwa Mungu kwa ajili ya watoto wake ni zetu (1 Wakorintho 3:22,23; Waefeso 1:3)

**MAKUHANI WA KIFALME** - Sifa ya tatu tuionayo ni kwamba wakristo ni makuhani wa kifalme. Kwa mujibu wa mtume Petro sisi ni ukuhani wa kifalme (1Petro 2:9). Kwa mujibu wa Yohana, tu wafalme na makuhani kwa Mungu (Ufunuo 1:6). Kama Wafalme na makuhani twapaswa kuitoa miili yetu kuwa dhabihu zilizo hai (Warumi 12:1). Hili ni tofauti kabisa na dhabihu za damu zilizotolewa chini ya mfumo wa kiyahudi.

**WAOMBEZI** - Sifa ya nne ambayo tunaipata ni kwamba Mkristo hutumika katika uwezo wa kuwa mwombezi, Pamoja na dua (maombi ya kujombea wenyewe), shukrani, na sala zingine, twapaswa kufanya sala za maombezi kwa ajili ya watu wote (1 Timotheo 2: 1,2). Kama wakristo tunatakiwa kuwaombea wakristo wenzetu (Waefeso 6:18-19)

**ASKARI** - Sifa ya tano tunayoiona ni kwama sisi kama Wakristo tunatazamwa na Mungu kama askari. Tunaweza tusijione hivyo kila wakati, lakini hilo halibadili ukweli kwamba sisi tu askari katika "jeshi la Mungu." Kama askari twapaswa kustahimili ugumu unaoambatana na uaskari (2 Timotheo 2:3). Kama askari lazima tuvipige vile vita vizuri (1 Timotheo 1:18). Kama askari wa Bwana tunatakiwa kuzivaa silaha zote za Mungu ili kujihami kwa kadri tunavyosonga mbele vitani (Waefeso 6:13-17).

**HEKALU** - Sifa ya sita tuionayo ni kwamba Wakristo hutumika kama hekalu la Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 3:16). Kama hekalu, Roho hukaa ndani yetu kwa njia ya neno la

Mungu lililoletwa na Roho Mtakatifu (Timotheo 3:16, 17). Kama makazi ya Roho Mtakatifu, tunatakiwa tuendelee kuwa watakatifu bila mawaa (1 Wakorintho 3:17)

**VYOMBO** - Sifa ya saba tunayoiona ni kwamba tunatakiwa kutoa miili yetu kwa Mungu kama vyombo vya haki (Warumi 6:13). Kila mmoja wetu, kama Wakristo, ni vyombo mikononi mwa Mungu (2 Timotheo 2:20, 21).

**VIUMBÉ VIPYA** - Sifa ya nane na ya mwisho tunayoiona ni kwamba tunatakiwa kuwa viumbé vipya katika ufalme wa Mungu. Lazima maisha yetu yote yawe yamebadilika kwa kumvaa Kristo (2Wakorintho 5:17). Kwa kilitazama badiliko hili, tunatakiwa kuenenda katika upya wa uzima (Warumi 6:4)

Kwa kuwa hatukiri kwa midomo tu kuwa Wakristo, na tutafute kuzitimiliza sifa hizi.